

*Picha ya kulia ni Mr. Mushi na mke wake (Joyce Mushi) wakifurahia jambo katika Kijiji cha Lionja B, Wilayani Nachingwea tarehe 07/07/2023 na picha ya kushoto ni Mr. Mushi akifurahia maandhali ya Mtwara tukiwa safarini kutoka Wilayani Tandahimba tarehe 10/03/2024.*

Kwa pamoja kama washirika wa Tujenge Nyumba ya Mungu tumekuwa tukiendesha huduma hii kwa kujitoa kwa mambo tofauti tofauti ikiwemo kuchangia gharama ya mafuta na matengenezo ya gari kwa wale wanaokwenda kubaini maeneo ya ujenzi huko vijijini na hivyo kusaidia kuwapunguzia gharama za safari (**Warumi 10:14-15).** Tunafanya hivi ili kulinda michango ile ambayo inakuwa imekusanywa ili itumike kwenye kusudi la ujenzi tu badala ya hizo kazi zingine za uendeshaji wa huduma.